

HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI

TAARIFA YA MRADI WA KUTENGENEZA MIKANDA YA GYPSUM USAGARA ILIYOTEKELEZWA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2018/2019.

1. MRADI WA KUTENGENEZA MIKANDA YA GYPSUM (KIKUNDI CHA VIJANA USAGARA)



Picha Na, 1: Jengo linalotumiwa na Kikundi cha Vijana wa Usagara kwa ajili ya Matengenezo na Kuhifadhaia Mikanda ya Gypusum, Kiwanda ambacho kilizinduliwa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2019.

Mradi wa kutengeneza mikanda ya Gypsum unatekelezwa katika Kijiji cha Idetemya Kata ya Usagara na ulianza tarehe **19/04/2018**

.Mradi huu unatekelezwa na kikundi cha Usagara Gypsum Group kilichosajiliwa kwa **namba 3747** ambacho kina jumla ya wanakikundi 5, kati ya hao vijana wa kiume wanne(4) na wa kike mmoja (1).

LENGO LA MRADI

Lengo la mradi huu ni kuwezesha vijana kujiajiri na kuinua vipato vyetu pamoja na kuhamasisha vijana kuwa wabunifu na kufanya kazi kwa bidii kwa maendeleo ya Taifa, ikiwa ni pamoja na kutekeleza na kuunga mkono Sera ya uanzishwaji wa viwanda ili kufikia Uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025. Uzinduzi wa mradi huu unatekeleza kigezo namba 4 kipengele cha 4.3 kinachohusu

“Halmashauri ilivyotenga na kuwakopesha vijana asilimia 4 ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2018/19”.

GHARAMA ZA MRADI

Mradi ulianza na mtaji wa Tshs **6,800,000/=** fedha hizi zilitokana na michango ya wanakikundi pamoja na faida iliyotokana na mradi wetu wa awali ambao ulikuwa ni kilimo cha mboga na matunda.

Hadi sasa mradi una mtaji wa Tshs **17,800,000/=** kati ya fedha hizo jumla ya Tshs **11,000,000/=** ni mkopo toka Halmashauri ya Wilaya Misungwi.

UZALISHAJI

Awali uzalishaji ulikua ni mikanda 50 kwa siku, hii ilitokana na ukosefu wa vitendea kazi pamoja na ufinyu wa karakana. Hadi sasa uzalishaji umeongezeka kutoka mikanda 50 hadi mikanda 250 kwa siku.

MAFANIKIO

- Kujiajiri hivyo kuondokana na adha ya kukosa shughuli ya kufanya.
- Kuwa na kipato cha uhakika kinachotusaidia kukidhi mahitaji yetu pamoja na ya familia zetu.
- Kuongeza uzalishaji wa bidhaa kutoka mikanda 50 hadi 250 kwa siku.
- Kukuza soko la bidhaa ambapo mikanda kwa sasa inauzwa ndani na nje ya Wilaya ya Misungwi Mfano Wilaya ya MAGU.

MIKAKATI/MATARAJIO

Matarajio katika mradi huu ni:-

- Kupanua mradi wetu kwa kuongeza uzalishaji wa bidhaa nyingine zinazazotumia malighafi ya Gypsum mfano Gypsum bodi na maua ya kona.
- Kuendelea kuitangaza bidhaa yetu ili tuweze kuhudumia wateja wa ndani na nje ya nchi.
- Kuwezesha ajira pamoja na mafunzo ya vitendo kwa vijana wenzetu ili nao waweze kufikia malengo yao.



Picha Na, 2 na Na, 3: Zinaonyesha namna Kikundi cha Vijana wa Usagara wanavyotengeneza Mikanda ya Gypsum katika Kiwanda kidogo cha Usagara Gypsum Group pamoja Mikanda hiyo iliyokamilika tayari kwa mauzo kwa Wateja .



Picha Na, 4: Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2019 Mzee Mkongea Ali akimpongeza Mwenyekiti wa Kikundi cha Vijana cha Usagara mara baada ya kuzindua shughuli za Kutengeneza Gypsum Kikundi cha Vijana wa Usagara wanavyotengeneza Mikanda ya Gypsum Kiwandani hapo.

Nawasilisha,

**Kisena Mabuba
Mkurugenzi Mtendaji (W)
MISUNGWI**